

# MIFUMO YA MBEGU INAYOSIMAMIWA NA WAKULIMA BARANI AFRIKA

**M**ifumo ya kilimo katika bara la Afrika inatokana na wakulima wadogo ambao hurudia kupanda na kubadilishana mbegu walizohifadhi kutoka kwenye mavuno yaliyopita. Mfumo huu wa mbegu unaosimamiwa na mkulima ni desturi ya miaka mingi kuanzia enzi za mababu zetu walipoanza kulima. Mfumo huu hutoa asilimia zaidi ya 80 ya mbegu zinazotumika katika kuzalisha chakula kwa mamia ya mamilioni ya Waafrika katika bara hili. Kwa mfano, katika nchi za Kusini mwa Afrika, wakulima wadogo hupata takribani asilimia 10 tu ya mbegu wanazotumia kutoka kwenye sekta rasmi/sekta ya biashara.

Kushirikiana na kubadilishana mbegu kunakofanywa na wakulima wadogo kumepokea kuwepo na anuwai kubwa ya mbegu na mazao. Uwepo wa uanuwai ni muhimu sana katika kuwasaidia wakulima kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, kama vile ukame wa muda mrefu. Pia hutoa lishe bora kwa watu na wanyama na kurutubisha udongo.

Wakulima wadogo ndio kundi kubwa zaidi la wazalishaji wa mbegu kwa miaka mingi. Wanachagua, wanahifadhi na kuendeleza mbegu, wakitafuta sifa kama vile kukomaa mapema, kustahimili ukame, ladha nzuri na sifa nyinginezo ambazo huhitajika kwa madhumuni ya kitamaduni. Ili kukidhi mahitaji yetu ya chakula na maisha ya baadaye, serikali zetu hazina budi kutambua, kusaidia na kulinda mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima.

